

TAARIFA KWA UMMA



WITO WA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA JKT KWA KUJITOLEA MWAKA 2023

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele, anawataarifu Vijana wote wa Tanzania Bara na Visiwani nafasi za kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa kujitolea kwa mwaka 2023.

Utaratibu wa Vijana kuomba na hatimaye kuchaguliwa kujiunga na mafunzo hayo, unaratibiwa na Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya ambako mwombaji anaishi. Aidha, vijana wenye Taaluma za Uhandisi wa Ujenzi (Civil Engineers), Ufugaji, Umwagiliaji, Uvuvi, Saikolojia na Wanyama pori wanashauriwa kujitokeza kwa wingi kupitia Mikoa yao.

Usaili wa Vijana hao kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa kujitolea utanza tarehe 28 Agosti 2023 kwa Mikoa yote Tanzania bara na Visiwani. Vijana wataochaguliwa watatakiwa kuripoti kwenye Makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa kuanzia tarehe 26 Septemba 2023 hadi 29 Septemba 2023.

Aidha, Jeshi la Kujenga Taifa linapenda kuwataarifu Vijana watakaopata fursa hiyo kuwa halitoi ajira, pia halihusiki kuwatafutia ajira katika Asasi, Vyombo vya Ulinzi na Usalama

na Mashirika mbalimbali ya Kiserikali na yasiyo ya Kiserikali, bali hutoa mafunzo ambayo yatawasaidia Vijana kujiajiri wenyewe mara baada ya kumaliza Mkataba wao na Jeshi la Kujenga Taifa.

Sifa za muombaji na maelekezo ya vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo ni kama ifuatavyo;

Sifa za Muombaji:-

1. Awe raia wa Tanzania.

2. **Umri.**

a. Kwa Vijana wenye Elimu ya Darasa la Saba umri ni kuanzia miaka **16** hadi **18**, waliomaliza Elimu ya Msingi kuanzia Mwaka **2020, 2021, 2022** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Msingi

b. Vijana wenye Elimu ya Kidato cha Nne umri usiwe zaidi ya miaka **20**, waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia Mwaka **2020, 2021, 2022** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate). Awe na ufaulu wa Daraja la Kwanza hadi Daraja la Nne. Kijana mwenye Daraja la Nne awe na ufaulu wa alama kuanzia **26** hadi **32**.


c. Vijana wenye Elimu ya Kidato cha Sita umri usiwe zaidi ya miaka **22**, waliomaliza Elimu ya Sekondari kuanzia Mwaka **2020, 2021, 2022** na awe na cheti halisi cha kumaliza Elimu ya Sekondari (Secondary Leaving Certificate) na cheti halisi cha matokeo (Academic Certificate). Awe na ufaulu wa Kuanzia Daraja la Kwanza hadi Daraja la Nne.

- d. Vijana wenye Elimu ya Stashahada umri usiwe zaidi ya miaka **25**, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.
- e. Vijana wenye Elimu ya Shahada umri usiwe zaidi ya miaka **26**, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.
- f. Vijana wenye Elimu ya Shahada ya Uzamili umri usiwe zaidi ya miaka **30**, awe na vyeti vya Sekondari na cheti cha Chuo.
3. Awe na Afya njema, Akili timamu na asiwe na alama yoyote ya michoro mwilini (Tattoo).
 4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.
 5. Awe na Kitambulisho cha Taifa au namba ya utambulisho Kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
 6. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (Original Birth Certificate).
 7. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo wala kuajiriwa na idara nyingine Serikalini.
 8. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma kwa **Kundi la Kujitolea** au **Kundi la lazima (Mujibu wa Sheria)**.
 9. Asiwe amejihusisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana na hayo.
 10. **Angalizo:** Kijana atakayepatikana na nyaraka za kughushi atachukuliwa hatua kali za kisheria kulingana na taratibu zilizopo.

JKT linawataka vijana hao kuripoti wakiwa na vifaa vifuatavyo:-

1. Bukta ya rangi 'Dark Blue' yenye mpira kiunoni (elastic) iliyo na mfuko mmoja nyuma, urefu unaoishia magotini isiyo na zipu, kwa vijana wa kike iwe na mpira kiunoni na kwenye pindo za miguu.
2. Raba za michezo zenye rangi ya kijani au blue.
3. Shuka mbili za kulalia zenye rangi ya blue bahari.
4. Soksi ndefu za rangi nyeusi.
5. Nguo za kuzuia baridi kwa waliopangiwa mikoa yenye baridi.
6. Truck suit ya rangi ya kijani au blue.
7. Flana ya kijani kibichi yenye kola ya duara isiyo na maandishi.
8. Nauli ya kwenda makambini na kurudi nyumbani.

Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele, anawakaribisha Vijana wote watakaopata fursa hiyo kuja kujiunga na vijana wenzao ili kujengewa Uzalendo, Umoja wa kitaifa, Ukakamavu, Kufundishwa Stadi za Kazi, Stadi za Maisha na utayari wa kulijenga na kulitumikia Taifa lao.



Handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Bug Gen'.

**Imetolewa na:
Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,
Makao Makuu ya JKT,
Tarehe 25 Agosti 2023.**